East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora

*Ibrahim Matin[1*] na Simiyu Kisurulia[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Rongo, S. L. P. 103, Rongo- Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030, Kericho- Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: matinibrahim40@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*27 Mei 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Ubunifu, Mwonoulimwengu, Mwingilianomatini.*

## IKISIRI

Katika kazi ya fasihi, mawazo, mafunzo na falsafa ya msanii hubainisha msimamo wake kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Msimamo ni ile hali ya mwandishi kuamua kufuata na kushikilia jambo fulani. Jambo hili huweza kukataliwa na wengi lakini akalishikilia tu. Msimamo ndio huweza kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaoandika kuhusu mazingira yanayofanana. Hili ambalo msanii anashikilia sana ndilo tunaloita katika utafiti huu kuwa mwonoulimwengu wa mwandishi. Ni vyema kujiuliza ni mambo gani yanayomsukuma na kuchochea mwandishi Ken Walibora kuchukua mawazo, msimamo na mkondo fulani katika uandishi wake. Uchanganuzi huu ulinuia kuchunguza mwonoulimwengu wa Ken Walibora kwa kujaribu kudokoa mawazo na falsafa zake kama zinavyojitokeza katika kazi zake za kisanaa. Huu ulikuwa utafiti wa maktabani ulioongozwa na nadharia za uhalisia na mwingilianomatini kuchunguza mwonoulimwengu wa Ken Walibora kupitia yale anayosema kujihusu na yale wengine wanasema kumhusu kisha kuyalinganisha na kazi za fasihi alizoandika kwa lengo la kuona mfanano wa mwonoulimwengu wake kwa sababu mwonoulimwengu unaonekana kutokana na maudhui yanayoendelezwa katika kazi za kisanaa. Kwa kutumia mbinu ya uteuzi sampuli maksudi tuliteua vitabu sita: Siku Njema (1996), Damu Nyeusi (2008), Kidagaa Kimemwozea (2012), Nasikia Sauti ya Mama (2014), Mbaya Wetu (2014) na Kisasi Hapana (2008). Tulivilinganisha ili kutambua mfanano wa mwonoulimwengu wa Ken Walibora katika vitabu hivi. Tulitathmini mwonoulimwengu huu kwa kujaribu kuelewa namna anavyosuka maudhui katika kazi zake kwa sababu mwonoulimwengu hudhihirika katika maudhui. Utafiti huu utachangia katika kufanyiza akili, kupanua uelewaji, kunoa nguvu za kufikiri, kupanua mwono, kukuza uwazaji na hisi ya ujumui ambalo ni lengo kuu la kazi yoyote ile ya fasihi. Wasomaji wa kazi za Ken Walibora watapata kuelewa kazi zake vizuri zaidi kwa kuwa na picha kubwa ya msanii huyu akilini. Pia inaweza kuwa kichocheo kwa wasanii wapya ili kujua namna ya kupata maoni ya kusuka kazi zao.

**APA CITATION**

Matin, I. & Kisurulia, S. (2024). Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 253-271. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

**CHICAGO CITATION**

Matin, Ibrahim and Simiyu Kisurulia. 2024. "Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 253-271. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954.

**HARVARD CITATION**

Matin, I. & Kisurulia, S. (2024) "Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 253-271. doi: 10.37284/jammk.7.1.1954

**IEEE CITATION**

I. Matin & S. Kisurulia "Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 253-271, May. 2024.

**MLA CITATION**

Matin, Ibrahim & Simiyu Kisurulia. "Ubunifu na Mwonoulimwengu wa Mwandishi: Mifano ya Kazi za Ken Walibora". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, May. 2024, pp. 253-271, doi:10.37284/jammk.7.1.1954.

## UTANGULIZI

Akiongea wakati wa sherehe ya kutolewa rasmi kwa tamthilia ya *Mbaya Wetu,* Hezekiel Gikambi, mwanahabari mashuhuri kutoka *Nation Media Group* katika gazeti la *Taifa Leo* la Jumanne 3 Juni 2014, alisema kuwa:

> *"Ajabu inatokea pale ambapo tunashuhudia baada ya wiki mbili tangu tamthilia hii ya Mbaya Wetu itolewe, takriban watu mia moja waliaga dunia, wengi kulazwa na hata wengine kupofuka kwa sababu ya unywaji wa pombe haramu katika maeneo mbalimbali nchini Kenya. Hii ni sadfa iliyoje? Mbona Walibora anaandika kuhusu jambo fulani na baada ya muda mfupi linatokea?*

Maneno haya yanaonyesha uhalisia na ukweli wa kazi za fasihi na hasa kazi za huyu mwandishi, Ken Walibora. Ingawa matokeo haya yaweza kuwa sadfa tu, yanaonyesha kuwa kazi za Ken Walibora zinadhihirisha mwonoulimwengu ulio na uhalisia mkubwa na kuna uwezekano wa yanayosawiriwa kutokea katika hali halisi. Kando na *Mbaya Wetu,* kuna mfano wa riwaya iliyojaa taharuki ya *Kufa Kuzikana* (2003) ambayo inasemekana kudhihirisha mwonoulimwengu wa kihalisia kupitia kwa matukio yake kama yalivyoshuhudiwa katika vita vya kikabila nchini Kenya ambavyo vilishuhudia vifo vya watu zaidi ya 1000 baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Mifano ya kabila la Wakanju na Wakorosho na uhusiano wa Akida na Tim unakuwa ni visa bainifu katika vita hivi vilivyotokea kikweli hapa nchini Kenya. Kitabu cha Ken Walibora cha watoto kiitwacho *Kisasi Hapana* (2009), kilichoshinda tuzo ya Jomo Kenyatta ya mwaka huo wa 2009, kilikuwa pia kama kiona mbele cha juhudi za maridhiano na kusameheana ambazo zilikita nchini Kenya baada ya mwaka huo. Hatimaye kitabu chake cha *Ndoto ya Amerika* na pia tafsiri yake *ya American Dream* vilitokea wakati wa hekaheka za mtu mweusi, Barack Obama, kuchaguliwa kuwa rais wa Marekani.

Kutokana na mawazo haya tunapata mshawasha wa kuchunguza mwonoulimwengu wa Ken Walibora katika kazi zake za kisanii. Hii ni kwa sababu mbali na kufurahisha, sanaa ina mvutano mkubwa katika maisha ya waja na hivyo kuathiri mitazamo na mienendo yao. Athari hii yaweza kuwa chanya au hasi na hivyo ikawa muhimu katika mustakabali wao. Ndipo Beck (1991) anasema kuwa usanii hautokani na ombwe tupu, usanii ni dhihirisho la maisha ya mwandishi na mwonoulimwengu wake. Hivyo katika fasihi na ubunifu wowote ule mwonoulimwengu wa msanii una umuhimu mkubwa kwa vile hatimaye unaigwa na kuathiri msomaji kwa kiwango kisicho na kifani (Wellek na Warren, 1949).

Mada hii ni ya maana kwa sababu kazi za Ken Walibora zimeteuliwa na kutumiwa katika taasisi za elimu mbalimbali ndani na nje ya mipaka ya nchi hii na hivyo kufikia hadhira pana sana. Jambo la pili ni kuwa kazi za msanii huyu zinaakisi maisha halisi kama yalivyo katika jamii yetu. Leland (1976) anaeleza kuwa msomaji anapaswa kusaidiwa kusoma akiwa na picha kubwa ya msanii na sanaa yake akilini. Hili ni muhimu kwa sababu ubunifu huhuisha kivuli cha uhalisia kutokana na udokozi wa mwonoulimwengu wa mwandishi. Kwa hivyo tunahakiki kazi hizi ili

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

kuelezea wasomaji wa Ken Walibora kile kinachoweza kuwa kinamwongoza katika kazi zake ili kumteka msomaji wake (Coombes, 1953). Hatimaye, kupitia mapitio yetu hatukupata ithibati kuwa uhakiki wa mwonoulimwengu wa waandishi umefanywa na hasa wa huyu msanii Ken Walibora. Kwa sababu mada hii haijachunguzwa sana tutafungua uwanja mwingine wa uhakiki ambao unaweza kuchangia katika kujenga ujuzi kwa ujumla.

## MISINGI YA NADHARIA

Kazi hii iliongozwa na nadharia za uhalisia na mwingiliano matini.

### Nadharia ya Uhalisia

Kulingana na Wamitila (2003), uhalisia ni mkondo wa uhakiki unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Nadharia hii inapigiwa upatu na George Lukacs ambaye ni mfuasi wa Marx. Nadharia hii ilizuka katika karne ya 19 hususan kwa sababu ya kupinga mkondo wa ulimbwende. Mihimili ya nadharia hii inashikilia kuwa fasihi inapaswa kusawiri uhalisi katika ukamilifu wake. Hii ina maana kuwa yanayoshughulikiwa katika kazi yoyote ile ya fasihi yanapaswa kuthibitika katika ulimwengu halisi. Kwa njia hii, uhalisia unaelekea kutilia mkazo mkubwa kwenye dhana za Kimimesia au kimuhakati ambazo husisitiza uwasilishaji ambao unakaribiana na mwigo wa moja kwa moja na unaoweza kuthibitishwa kwa tajriba. Kwa njia hii msanii anaweza kuteua habari lakini iwe bila kupiga chuku. Tuliongozwa na mhimili huu katika kuteua mwonoulimwengu uliosawiriwa katika vitabu tulivyochunguza. Mwonoulimwengu huu ni yale mawazo yanayoweza kutokea au hata yaliyotokea tayari na yanaweza kuthibitishwa kwa mifano. Hasa mwonoulimwengu katika *Nasikia Sauti ya Mama* ni mambo yaliyotukia kweli kutokana na uelewa kuwa kazi hii ni tawasifu na hivyo ni masimulizi ya yale yaliyotukia kweli.

Mhimili wa pili unasisitiza kuwa lazima kuchunguza undani wa picha inayoonekana ya uhalisia na kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazosababisha hali fulani. Mhakiki au mwandishi anayeongozwa na nadharia hii ana jukumu moja muhimu la kuuelewa ulimwengu kama kitu changamano na kinachobadilika. Kwa hivyo anapaswa kuzifichua sheria au kani zinazosababisha haya mabadiliko katika kazi yake. Tulitumia mhimili huu kuchunguza tawasifu ya Ken Walibora ya *Nasikia Sauti ya Mama* kutambua mambo ambayo anasimulia yeye mwenyewe na yanayoweza kuwa yanaathiri jinsi anavyoona ulimwengu. Mambo haya bila shaka yana athari kubwa katika yale anayoangazia katika kazi zake nyingine.

Pia, mhalisia humwona mhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi ya fasihi na hivyo saikolojia ya wahusuka inapaswa kuzingatiwa katika hadithi. Mhimili huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa wahusika wametajwa katika kazi zote tulizokuwa tunatathmini. Mhimili huu ulitusaidia kutambua kuwa wahusika waliotajwa na mwandishi huyu wamewekwa katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi. Baadhi ya majina na tabia zao ni zile zilizotajwa na mwandishi katika tawasifu yake. Hili linamaanisha kuwa picha za ulimwengu alizoumba msanii huyu si mambo ya kihisia na yasiyo halisi maishani (Ntarangwi, 2004).

Kwa hivyo uhakiki unaoegemea mkondo wa nadharia ya uhalisia unamtarajia msanii wa kazi ya fasihi aweze kusawiri wahusika, matukio mbalimbali, mandhari ambayo yanakubalika na yanayoweza kuaminika katika jamii ya wakati wake. Ili kutimiza hili, msanii huyu basi anahitaji kuelewa vizuri mazingira na maisha ya wale anaowalenga katika kazi yake ya utunzi. Mhakiki kwa upande wake bila shaka atahitaji kuelewa mwandishi na mazingira yanayomzunguka pamoja na kazi yake ili kutokeza mwonoulimwengu wake. Kwa kuongozwa na wazo hili ilibidi watafiti watafute habari mbalimbali kuhusu maisha ya mwandishi huyu Ken Walibora ili kumwelewa kindani zaidi.

Hata hivyo watafiti wa kazi hii wanakubali kuwa nadharia hii ya uhalisia ina utata kwa kiasi fulani kwa kuwa uhalisia si jambo rahisi mno na lisilo na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

ugiligili fulani katika jamii yoyote ile. Pia ni muhimu kukubali kuwa kila mmoja katika jamii yoyote ile huona uhalisia katika njia yake na iliyo tofauti kabisa na yule mwingine.

**Nadharia ya Mwingilianomatini**

Kulingana na Allen (2000) na Raj (2015) neno 'mwingilianomatini' liliasisiwa na mwananadharia Julia Kristeva katika miaka ya 1960 kwa kuathiriwa na dhana ya Bakhtin ya usemezano ambapo wote waliamini kuwa semi kutoka kazi mbalimbali huhusiana na kuingiliana ili kukamilishana kimaana. Matini moja haiwezi kujitosheleza bila kuhusishwa na matini nyingine inayohusiana. Waendelezaji wa nadharia hii wanaamini kuwa maana ya matini inayoundwa huweza kuwa na maana pana zaidi kuliko ile inayopatikana kwenye matini yenyewe. Wanazidi kushikilia kuwa maana inayoibuka lazima ieleweke katika muktadha wa jamii ambamo kazi ya sanaa hubuniwa. Na pia kila matini za kifasihi kwa njia moja au nyingine huchota, hunukuu, hugeuza, huiga au kurejelea matini nyingine kwa njia moja au nyingine na kwa misingi hii matini mpya huweza kubadili au kuleta maana mpya mbali na ile ya awali. Hii ndiyo sababu katika utafiti huu vitabu sita vya Ken Walibora vinachunguzwa pamoja kwa kulinganishwa ili kuonyesha mwonoulimwengu unavyoingiliana katika kazi hizo.

Wamitila (2002) anashikilia kuwa kazi ya kisanaa hasa fasihi katika muktadha wa mwingilianomatini haiwezi kujitegemea yenyewe kimaana bali inahitaji kupata urejelezi wa kazi nyingine hasa ya awali katika misingi ya mwingiliano wa mitindo ya uashiriaji. Hii ina maana kuwa hata mwandishi mmoja ambaye ameandika kazi kadhaa huwa anaathiriwa katika uandishi wake na mwangwi wa kazi zake za awali na hivyo kutokeza dhana ya usemezano kati ya kazi hizo. Kwa jinsi hii matini kadhaa huweza kuingiliana kwa misingi ya mandhari, wahusika, maudhui, mtindo, dhamira na hata mwonoulimwengu. Kwa kuongozwa na wazo hili, mwonoulimwengu wa Ken Walibora unaweza kueleweka kutokana na kuchunguza kazi zake kadhaa. Hili linaweza kutimizwa kwa kuchunguza kazi za aina mbalimbali na zilizoandikwa kwa kipindi fulani kirefu. Kazi hizi licha ya kuwa za tanzu tofauti na zilizoandikwa kwa kipindi fulani zinasemezana. Kupitia kwa usemezano huu unaotokana na tofauti za mfumo wa lugha na utamaduni, tunaweza kuelewa mwonoulimwengu wa mwandishi wa kazi husika. Katika kisa hiki ni mwonoulimwengu wa Ken Walibora.

## MBINU ZA UTAFITI

Katika kuandaa makala haya, utafiti ulifanywa maktabani na ulihusisha uchanganuzi matini. Katika uchanganuzi matini kuna mambo kadhaa yaliyohusika ambayo ni kusoma kwa undani vitabu vya Ken Walibora, magazeti, matini, makala, tasnifu, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizomo maktabani na mtandaoni na hivyo tukapata habari za kina (Kothari, 2008). Idadi jumla ya utafiti huu ilikuwa ni makala na vitabu vyote vilivyoandikwa na Ken Walibora. Kazi hizo ni nyingi. Hata hivyo kwa mujibu wa makala haya utafiti huu uliongozwa na maoni ya Neuman (2006) na Gall na wenziwe (1996) wanaosema kuwa uteuzi sampuli kimakusudi humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayomwezesha kujibu maswali ya utafiti kwa kuwa ina data ya kutosha na inayohitajika hasa katika utafiti wa kithamano. Kwa kuongozwa na maoni haya watafiti waliteua *Siku Njema* (1996), *Damu Nyeusi* (2008), *Kidagaa Kimemwozea* (2012), *Nasikia Sauti ya Mama* (2014), *Mbaya Wetu* (2014) na *Kisasi Hapana* (2008). Pia, watafiti walipitia makala mbalimbali ambayo Ken Walibora aliwahi kuandika kuhusu maswala mbalimbali. Tuliteua kazi hizi kimakusudi kutoka katika kazi za miongo mbalimbali. Hii ni kwa sababu ili kuelewa mwonoulimwengu wa mtu lazima kumchunguza kwa kipindi kirefu iwezekanavyo (Wamitila, 2003).

Tuliwasilisha data ya mwisho kithamano kwa kuzingatia maoni ya Truex (1996) ambaye anaeleza kuwa uchanganuzi matini kithamano humpa mtafiti nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele vya umbuji wa sanaa na maana inayojitokeza katika vipengele hivyo vya sanaa hiyo. Katika muktadha huu vipengele vya umbuji

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

wa sanaa ni mwonoulimwengu ambao unajengwa kwa kulinganisha kazi mbalimbali za mwandishi kwa kipindi fulani cha muda ili kutokeza mwonoulimwengu wa mwandishi kwa njia wazi zaidi.

## MAANA YA MWONOULIMWENGU

Kulingana na American Heritage Dictionary (2000) neno mwonoulimwengu linatokana na neno la Kijerumani *Weltanschauung*. Lilitumiwa kwa mara ya kwanza na Kant kisha Hegel. Neno hili lina maana ya imani, filosofia, msimamo, utamaduni au mtazamo wa jumla unaoshikiliwa na mtu na ambao humwezesha kuutazama ulimwengu wake kutokana na tajriba ya mda mrefu.

Sire (2010) anafafanua mwonoulimwengu kuwa uwajibikaji au mwelekeo wa moyo wa kweli au usio wa kweli unaoshikiliwa na mtu fulani kwa kujua au kwa kutokujua. Mwelekeo huu huonyesha maoni ya mtu kuhusu uhalisi na humwekea msingi wa kuishi. Inahusu uelewaji wa uhalisia, mkusanyo wa mawazo, mielekeo kuhusu ulimwengu, itikadi, maadili, tabia, furaha, imani na tajriba ya maisha. Husaidia kujibu maswali kama binadamu ni nani? Kwa nini tupo hapa? Maisha yana kusudi gani? Maadili yetu ni yapi? Mwonoulimwengu huu husaidia mtu kutambua yaliyo mema, matakatifu, yaliyo kweli na halisi (Hill, 2019).

Mtazamo mwingine ni wa Wamitila (2003), anayesema kuwa mwonoulimwengu ni dhana inayohusishwa na mhakiki anayeitwa George Lukacs. Mhakiki huyu anaitumia dhana hii kuelezea mtazamo maalum wa mwandishi kuhusiana na masuala anayozungumzia katika kazi yake na kuwa kila mwandishi ana njia yake maalum ya kutazama ulimwengu, hali na matukio mbalimbali. Bila shaka ili kusema kuwa huu ni mwonoulimwengu wa mwandishi lazima kuwe na idhibati kuwa hiyo ndiyo ruwaza anayoiendeleza katika uwazaji na uandishi wake. Ni mkusanyo wa imani ambazo mtu huwa nazo kuhusu maswala muhimu ya maisha kama Mungu, ulimwengu (cosmos), ujuzi, maadili, siasa, dini, ubinadamu na historia. Wanafananisha mwonoulimwengu na miwani ambayo humsaidia mtu kuuelewa ulimwengu unaomzunguka na kuwa miwani hii huweza kuonyesha ulimwengu kwa njia nzuri au hata kwa njia iliyopotoka. Ili kuthibitisha mwonoulimwengu huo ni lazima kupitia kazi kadhaa ili kuonyesha kuwa ni mwelekeo usiokanika wa mtu huyo. Kwa hivyo, ni wazi kuwa yale anayoyapigia debe mwandishi katika kazi yake ya sanaa huwa yana uwezekano mkubwa kuwa ndiyo msimamo wake, falsafa yake, na mwonoulimwengu wake kuhusu jambo au hali na ndilo angependa ikiwezekana liigwe na msomaji wake (Samples, 2007, Spirkin, 1990).

Ntarangwi (2004) anasema kuwa mwandishi hufanya kazi yake sawa na mtoto anayecheza pale ambapo yeye huumba ulimwengu wake bunia kwa kuutilia maanani sana huku akiutenganisha na uhalisia. Ili kuumba ulimwengu huu bunifu mwandishi hutumia visa halisi vya maisha na kuunda ulimwengu huu bunia ambapo mambo anayozungumzia huwa ni yanayoweza kutokea. Visa hivyo anavyoumba huweza kuwa vile ambavyo yeye mwenyewe amepitia au anatamani au anachukia na kwa njia hii kubuni mwonoulimwengu wake. Ntarangwi anazingatia nadharia ya Sigmund Freud anayeona kuwa kazi ya fasihi inapaswa kuchukuliwa kuwa kielezo cha matamanio ya mtunzi na juhudi zake za kuyatimiza katika ulimwengu wa sanaa. Kwa hivyo inabidi mhakiki kwa kiwango fulani azingatie maisha halisi ya mtunzi husika ili kuielewa kazi yake ipasavyo. Hii ndiyo sababu ili kuelewa mwonoulimwengu katika kazi za Ken Walibora, utafiti huu unarudi nyuma kabisa na kupitia maisha yake kwa kiasi fulani na kwa kufanya hivi inakuwa rahisi kumwelewa vizuri zaidi na hivyo kuwa na picha kubwa akilini wakati wa kupitia na kusoma kazi zake za kisanii. Ili kutimiza hili mwandishi huchora wahusika walio na itikadi, imani, mtazamo, utatuzi wa matatizo, asili, maana ya ulimwengu, falsafa, msimamo, mtizamo wa kidini, kisiasa na kisayansi ili wakubalike katika utunzi wake na kwa wasomaji wake pia.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa ni wazi kuwa mambo anayopitia msanii maishani huamua

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

na kujenga mwonoulimwengu wake na hatimaye huwa na athari kwa sanaa yake. Kwa hivyo mwonoulimwengu wa msanii huweza kudhihirika katika yale watu wanasema kumhusu na kazi zake za kisanaa. Kwa sababu hii inatubidi tujiulize ni mambo gani aliyopitia Bwana Ken Walibora yanayoweza kuwa yana athari kwake na kujenga mwonoulimwengu wake? Mwonoulimwengu wa Ken Walibora unadhihirikaje wazi katika kazi zake za kisanaa? Hili ndilo swali ambalo utafiti huu ulinuia kujibu.

**Maisha ya Ken Walibora**

Kulingana na Bertoncini (2007), Ken Walibora alizaliwa Januari 1965 na alikulia Kitale Magharibi mwa Kenya katika Kaunti ya Tranzoia katika mkoa uliokuwa wa Bonde la Ufa. Baada ya kumaliza shule ya upili alifanya kazi ya maswala ya kijamii katika kitengo cha magereza kwa miaka minane. Jina lake kamili ni Kennedy Waliaula lakini alibuni jina la kutumiwa katika uandishi kwa kuondoa silabi za “aula”. Hii silabi katika Kiluhya na Kiswahili inaamanisha zuri au bora na hivyo akaibadilisha na bora ambalo ni neno linalotumika sana.

Ken Walibora mwenyewe anazungumzia maisha yake kindani tangu utotoni katika tawasifu yake ya *Nasikia Sauti ya Mama* (2014). Akizungumza katika mahojiano, Walibora alisema kuwa nyanya yake Sarah Kusimba alipenda sana kumsimulia hadithi na alijua sana kugana hadithi kwa njia ya kusisimua. Mama yake Ruth Nasambu Makali alizoea kumsimulia hadithi za Biblia kwa njia ya kupendeza na alikubali kuwa Biblia ilikuwa ni kitabu alichokipenda sana. Baba yake alikuwa mwalimu mkuu katika shule aliyoisomea naye pia alikuwa msimuliaji hadithi mwenye kufana. Walibora anakubali kuwa kukulia kwake katikati mwa hawa wasimuliaji wa hadithi kulimchochea sana awe na azma ya kusimulia hadithi kwa njia fulani. Yeye pamoja na ndugu zake Arthur, Eunice na Patrick walipenda sana kusoma na baba yao alihakikisha kuwa wana vitabu vya kutosha vya kusoma (Walibora 2014).

Naibu mwalimu mkuu katika shule ya msingi ya Suwerwa alikosomea pia alimsaidia kupata vitabu na anataja kihususa kuwa baadhi ya vitabu alivyopata kusoma mwanzoni vilitia ndani *Adili na Nduguze*, *Hekaya za Abunuasi* na *Robert Loouis Stevensons Kidnaped*. Baadaye maishani alisomea shule ya upili ya Olkejuado. Anasema katika shule hii alipenda sana kandanda na alikuwa mlinda lango bora sana. Katika shule hii pia aliandika makala katika jarida la shule kila mara. Mara kwa mara alichora ili kudhihirisha ubunifu wake na uwazaji wake kuhusu mambo. Alikuwa na marafiki ambao walipenda sana fasihi na kwa njia moja au nyingine walimwathiri ili kufikia lengo lake. Baadhi ya marafiki hawa ni Josiah Momanyi, James Njiru, Kisaka Sakari, na Ben Bella Otieno. Wakiwa pamoja na marafiki hawa walipitia vitabu vya fasihi kama *The River Between cha Ngugi*, *No longer at Ease* cha Chinua Achebe, *Land without Thunder* cha Grace Ogot na *Poems from East Africa* cha David Cook. Wakiwa pamoja na rafiki yake Kisaka waliandika mashairi kwa wingi. Katika shule hii pia alikuwa na marafiki waliomtia moyo kufikiria kuwa mwandishi. Hao ni Alice Obuya na mwalimu mkuu wa shule hii ya Olkejuado Bwana Eliud Simiyu (Bertoncini 2007).

Baadaye pia alisoma katika shule ya Koelel na alisomea Fasihi ya Kiingereza, Kiswahili na Historia. Katika shule hii alionjeshwa fasihi za Urusi, India, Amerika, Uingereza na visiwa vya Karibian. Anakiri katika shule hii pia alipenda kandanda sana na akawa kiranja wa michezo. Hapa ndipo alipokutana na wale ambao walimchochea sana. Hawa ni Judy Ghikas, Alex Ngure, Ndachi M Ndachi na John Kundu. Kwa mfano Kundu alimwambia angeishi kwa kuandika vitabu naye Ngure aliwasimulia jinsi mswada wake ulivyokataliwa. Kufikia kidato cha sita alikuwa ameandika miswada kadhaa ingawa baadhi yake imepotea. Aliandika mswada wake wa kwanza akiwa katika kidato cha pili. Baada ya kuingia katika chuo cha Kenya Institute of Administration Geofrey Kinambuko Lukalo na Clement Oketch walishangazwa na uwezo wake mkuu wa uandishi na wakamdokezea kuwa alikuwa amechukua taaluma isiyofaa kwa kusomea utawala katika idara ya magereza.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

Baada ya kufuzu aliajiriwa kama afisa wa kiutawala katika idara ya magereza kati ya 1988 hadi 1996. Katika kipindi kile akifanya kazi katika kitengo cha magereza ndipo alipoandika Riwaya yake ya kwanza *Siku Njema*. Bertoncini (2007) anazidi kusema kuwa hata akiwa katika chuo cha usimamizi alitamani sana kazi ya utangazaji. Alijiunga na shirika la KBC kama mtangazaji katika mwaka wa 1996. Baadaye alirudi shuleni akiwa bado anafanya na shirika la KBC na akasomea Fasihi na Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi. Katika mwaka wa 1999 alianza kazi ya utangazaji rasmi na akajulikana kama mtangazaji bora sana wa televisheni. Baadaye alifuzu na shahada katika Fasihi na Kiswahili kutoka katika Chuo Kikuu Cha Nairobi. Katika mwaka wa 2004 alipata nafasi ya kusomea uzamili na uzamifu katika Fasihi ya Kiafrika katika chuo cha Ohio State kule Marekani. Baadaye hadi kifo chake alifanya kazi na shirika la utangazaji la Nation kama mkurugenzi katika kitengo cha ubora.

Kulingana na Bertoncini (keshatajwa) Walibora alikuwa akionwa kuwa kati ya waandishi na watangazaji bora sana nchini Kenya. Walibora alikuwa na ukwasi mkubwa katika lugha ya Kiswahili na alikuwa na sehemu kubwa katika kujenga na kuimarisha utangazaji katika lugha ya Kiswahili na hasa utafsiri wa habari kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Maswala haya yalitusaidia kusuka mwonoulimwengu wa Ken Walibora. Yale aliyojionea, watu aliotagusana nao na kazi alizofanya bila shaka yalikuwa na athari fulani kwake na jinsi alivyoona na kusawiri ulimwengu wake katika kazi zake za kiubunifu na hivyo kuchangia katika kujenga mwonoulimwengu wake.

**Mwonoulimwengu wa Ken Walibora Katika Kazi Zake za Fasihi**

Katika kudokoa mwonoulimwengu wa Ken Walibora kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia tulidondoa mwonoulimwengu wake katika *Nasikia Sauti ya Mama* kwanza kwa sababu hii kazi inahusu maisha yake halisia. Kisha kwa kuongozwa na nadharia ya mwingiliano matini tukadondoa mwonoulimwengu wa Ken Walibora kutoka katika kazi zake nyingine na kuulinganisha mwonoulimwengu huo na ule unaodhihirishwa katika *Nasikia Sauti ya Mama*. Mwonoulimwengu wake unaonekana kutokana na maudhui yanayoendelezwa katika kazi zake. Kazi hizi zimechukua tarkriban miongo miwili hivi kuanzia bunilizi yake ya kwanza ya *Siku Njema* (1996) hadi *Mbaya Wetu* (2014).

***Mwonoulimwengu Wa Ken Walibora Kuhusu Utu***

Ken Walibora katika *Nasikia Sauti ya Mama* anakiri kuwa mamake alikuwa akimwelekeza kila mara kutenda matendo ya kiutu katika maisha yake. Anasema hivi; "Naam tenda mema ujiepushe na mawi, ndio uliokuwa mkarara wa mama wa shairi lake alilonikariria kila uchao" (ukur. 38). Babake Ken Walibora, kwa kuongozwa na utu, alimwokota mpita njia mmoja kwa jina Henry Machelesi aliyekuwa amekondeana na alikuwa na njaa sana (kur. 66-67). Alimpeleka nyumbani kwake na kuwaamuru wamwandalie chakula. Baadaye Machelesi akaja kuwa mfanyakazi wao wa nyumbani hadi alipotoweka siku moja. Tunaelezwa pia kuwa nyumba zao kule Kitale mjini na shambani Sangura zilijaa wageni waliokaribishwa siku zote na wazazi wao.

Visa hivi vya kiutu vilichonga mwonoulimwengu wa Ken Walibora kwa kiwango kikubwa kwa sababu maudhui ya vitendo vya utu yanajitokeza kwa njia pana katika kazi zake za kifasihi. Kwa mfano katika *Kidagaa Kimemwozea*, Amani anaenda Sokomoko kutafuta waliomdhulumu kwa kuua mamake, kuwanyang'anya shamba na kumwibia mswada bila nia ya kulipiza kisasi. Akiwa njiani Amani anampa DJ shati baada ya kaputura yake kuliwa na fahali. Kisha naye DJ anafanya kitendo cha kiutu kwa kujitolea kuwapeleka Amani na Imani kwa Nasaba Bora na Majisifu mtawalia ili kutafuta ajira. Baada ya kufika Sokomoko, kwa kuonyesha utu wa hali ya juu, Amani anakichukua kitoto alicholazimishiwa na Mtemi licha ya kuwa hakujua kilikotoka na pia hakuwa na uwezo wa kukitunza. Anapoona hili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

Bi. Zuhura, kwa kusukumwa na utu, anamkumbusha mumewe Nasaba Bora kwamba akiwa mtemi ana wajibu wa kukipa hifadhi kitoto kilichotupwa mlangoni pa Amani. Mtemi anapokataa kumsikiliza, Bi Zuhura anaendelea kuwasaidia akina Amani na Imani kwa hali na mali kukilea kitoto Uhuru. Imani naye kwa kusukumwa na utu anajisababishia kuacha kazi kwa Majisifu kuja kumsaidia Amani kumtunza Uhuru. Huyu Imani akiwa angali kwa Majisifu, tunaambiwa kuwa anawalea watoto walemavu wa Majisifu kwa kuwaonea huruma. Kwa kufanya hivi, anabadili mtazamo wa Majisifu kuwahusu watoto walemavu.

Katika riwaya ya *Siku Njema* mwandishi anazidi kutufunulia mwonoulimwengu wa kiutu kwa kutuchorea mhusika Kongowea ambaye alikuwa ameabiri chombo cha baharini kwa jina MV Tawafiq kutoka Tanga kwenda Mombasa kutafuta babake. Akiwa chomboni alipoteza pesa zake pamoja na risiti ya nauli. Alipoulizwa na mkaguzi wa mle chomboni hakuipata stakabadhi hiyo kisha mkaguzi akamshika ukosi wa shati na kumzaba kofi. Mwandishi anasema:

"Amina alipoona hivyo, alifungua pochi yake na kutoa ndani shilingi hamsini na kumpa yule mkaguzi. Akamsihi azichukue kama nauli ya Kongowea. Yule mbilikimo akazitwaa na kuziweka mfukoni" (ukur. 51).

Walipofika Mombasa, Amina alimkaribisha kwake na kumtunza vizuri. Baadaye Kongowea alipata mhisani mwingine kwa jina Rashid. Huyu naye aliishi na Kongowea kama ndugu yake wa toka nitoke hadi kulipomharibikia na kuondoka kwenda Kitale (ukur. 61). Hivi ni vitendo vya kiutu anavyoshabikia mwandishi huyu.

Katika *Damu Nyeusi* Walibora anatashtiti ukosefu wa utu wa Fiona ambaye ni msichana mweusi anayekutana na Fikirini mweusi mwenzake baada ya kuachwa na basi la shule. Fiona anamdanganya Fikirini kuwa atamsindikiza shuleni kwa gari lake. Lakini anaishia kumpokonya kila kitu akisaidiwa na rafiki yake Bob. Huu ni ukosefu wa utu. Hata hivyo mwandishi anatumia kisa hiki kukashifu tabia ya Fiona na Bob (ukur. 26). Hii ni ishara kuwa mwandishi hashabikii tendo hili la ukosefu wa utu na hivyo si mwonoulimwengu wake.

Kido siku moja anakuwa mgonjwa kulingana na *Kisasi Hapana* na nyanyake pamoja na mamake wakaamua kumpeleka hospitali kwa kumbeba na kutembea kwa miguu kwa kilomita kumi na saba hivi. Hata hivyo wanapofika huko wahudumu wanaonyesha ukosefu wa utu kwa kupitisha marafiki zao wapate tiba huku Kido akiwa hatarini. Baada ya kuona daktari anakosa kupewa dawa kwa sababu ya ukosefu wa pesa na kulazimika kuelekea nyumbani licha ya hali yake kuwa mbaya zaidi. Wakiwa njiani Kido anazidiwa na wanalazimika kumlaza chini kidogo apumzike hadi usiku unawapata pale. Kwa bahati nzuri wanaona taa za gari na kulisimamisha ili wakasindikizwe nyumbani na mgonjwa wao. Hata hivyo Kido anaripoti hivi:

> *"Taa za gari zipotumulika nyanya aliinuka na kwenda kwenye ukingo wa barabara. Akampungia dereva mkono. Gari likaja na kusimama karibu naye. Dereva alitoka ndani akiwa na hasira tele. Akasema ondoka barabarani we wazimu wewe. Usituletee wazimu wako we bi kizee. Basi nilishtuka sana nilipomwona dereva yule anavua mkanda wake wa suruali. Halafu ghafla bin vuu akaanza kumtandika nyanya kwa mkanda wake. Alimtandika tena na tena. Nyanya akajiondokea huku analia kwa sauti kubwa. Kisha gari likaondoka na kujiendea zake."* (Kur 7-8).

***Uongozi Bora***

Viongozi katika *Kidagaa Kimemwozea* wanaendeleza wizi wa mali ya umma na kuwaua raia. Kwa mfano Mtemi Nasaba Bora ananyakua mali ya Chichiri Hamadi na Mwinyihatibu Mtembezi kisha anatuma watu kumuua Chichiri Hamadi ili aweze kunyakua shamba lake. Baadaye anatumia mahakama kufanikisha masilahi yake kwa kusingizia kuwa Yusufu ndiye aliyeua baba yake ili kumkinga na kumhifadhi Nasaba Bora na rafiki zake. Manesi wanatumia cheo vibaya kwa kukataa kukitibu kitoto Uhuru na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

kusababisha kifo chake. Mtemi Nasaba Bora anatumia mamlaka yake vibaya kwa kupagaza Amani kile kitoto Uhuru. Viongozi wengine serikalini wanawanyima vigogo wa vita vya kwanza haki yao. Kwa mfano Matuko Weye aliyetumika jeshini anaishi maisha ya kimaskini bila tumaini lolote kuwa hali yake itaboreshwa. Mudir wa wilaya alitumia cheo chake visivyo kwa kumpagaza Nasaba bora uongozi wa jimbo la Sokomoko ambalo hakustahili kupewa.

Vyombo vya dola vinatumiwa vibaya na viongozi wa mtemi Nasaba Bora kwa mfano askari wanatumiwa kuwafukuza Imani kutoka shambani mwao. Amani na Imani wanafungwa gerezani kwa kusingiziwa kuua kitoto Uhuru bila uchunguzi kufanywa ili kuthibitisha tuhuma hii. Mtemi Nasaba bora alionelea ni bora wafungwa kama Amani, Imani na Matuko Weye kuteswa gerezani badala ya kufikishwa kortini. Aliwaambia askari wake wakawafanyie kazi kama kawaida. Kwa upande mwingine, uongozi wa shule unakosa kumchukulia Mwalimu Majisifu hatua za kinidhamu kwa sababu ya kufika kazini akiwa mlevi na kutohudhuria vipindi vyake. Pia, idara ya elimu haichukui hatua wakati Fao anapofanyiwa mtihani wa darasa la nane na kidato cha nne.

Visa hivi vyote vinatoa mifano ya uongozi mbaya ambao unaenda kinyume na msimamo wa mwandishi. Anavikashifu na kuvipiga vita akidhamiria kuwa kuwepo na uongozi bora katika nyanja zote za maisha.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu,* swala la uongozi mbaya linaendelezwa kupitia kwa ufisadi katika idara ya polisi. Polisi wanapewa hongo ili kubatilisha haki. Kwa mfano, Mtu wa II anaambia Fiona:

> *" Na hata kama humjui huyu polisi kwani hicho ni kitu kwako wewe Fiona...Ghalibu hukosi chochote cha kumlainisha moyo wake yabisi. Askari wote lao moja…yaani bora mkono wende kinywani basi…" …Mzee Temba, nimekujia kadha si kadha wa kadha. Hebu sikiliza. Watu wa Jefule wamenituma nije niseme nanyi. Wako radhi kulipa fidia kesi imalizike papa hapa kijijini isiende mahakamani mjini"* (Ukur. 62).

Kupitia kwa kauli hizi inadhihirika wazi kuwa kuna uongozi mbaya katika idara ya polisi kwa sababu wanataka hongo ili kubatilisha haki. Fiona anataka kesi ifanywe nyumbani ndipo waliokosa wasipate adhabu waliyoistahiki. Ili hili litimie inambidi kutoa hongo ili kulainisha nyoyo za askari. Mwandishi anakejeli swala hili kuwa halifai. Linaharibu uongozi bora katika idara ya polisi.

### *Mwonoulimwengu Wa Ken Walibora Kuhusu Maadili*

Walibora mwenyewe anakiri katika *Nasikia Sauti ya Mama* kuwa alikuwa na msingi dhabiti wa kidini aliopata kutoka kwa nyanya yake na wazazi wake. Katika utafiti huu imebainika kuwa wosia wa mamake na nyanyake kuhusu maadili ya kingono uliathiri mwonoulimwengu wa mwandishi huyu. Hili linaweza kuwa limeathiri msimamo wake kuhusu maadili ya mahusiano baina ya mwanamme na mwanamke kama inavyodhihirika katika kazi zake. Wakati mmoja akiwa katika shule ya msingi baada ya kutahiriwa, msichana mmoja kwa jina Mariamu alimrai ili wajiingize katika mahusiano ya kingono. Kutokana na nidhamu aliyopata kutoka kwa mamake alishindwa kukubali ingawa kwa shingo upande. Katika *Nasikia Sauti ya Mama,* anasema hivi:

> *"Nataka nione kama kweli umechongwa kalamu au bado umebeba filimbi hapo katikati…. Nami pia nilitaka kuuvuka upande mwingine wa barabara, upande alioniambia mama unapaswa kusubiri hadi huku mbele wakati wa kufunga ndoa safi…Mpaka leo niandikapo haya nakisikia bayana kicheko kingine kikubwa zaidi cha baada ya ngoma. Kicheko cha Mariamu chapigana dafrao na sauti ya mama ninayosikia ikionya dhidi ya kuzifuata hawaa za ujana. Jidhibiti mwanangu usidhibitiwe".* (Kur. 129-130)

Baadaye alipoanza kuwa gwiji katika uandishi wa insha akiwa katika darasa la nane, akakumbuka

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

jinsi hisia zilivyomsukuma ili amwandikie msichana kwa jina Alice Hopf barua. Anakiri alimtamani kimapenzi kiasi cha kumuota na kuwa na njozi za matamanio. Hata hivyo kuna kitu kilichomzuia. Katika *Nasikia Sauti ya Mama* Anasema: “Lakini nasikia sauti ya mama ikisema, ‘Jidhibiti mwanangu usithibitiwe’. Laiti nisingekuwa na uwezo wa kuisikia sauti hii ya mama. Najirudi mwenyewe. Makosa yangu mengi, sitaki kuongezea mengine mengi” (Ukur. 137).

Ni dhahiri kuwa visa hivi na mashauri aliyopata katika maisha yake ya awali yalikuwa na athari kubwa juu ya mwonoulimwengu wake kuhusu suala la maadili ya mapenzi. Kwa mfano katika tamthilia ya *Damu Nyeusi* katika hadithi yake ya *‘Damu Nyeusi’* Fiona anamwambia Fikirini:

> *“Yule uliyemwona ni ndugu yangu…. Usiwe na wahka. Ndugu yangu nami twaishi pamoja hapa. Tunaelewana sana. Huwa hajishengeshi kwenye mambo yangu. Nami siyaingilii yake. By the way do you want a good time? Hapa ukumbini patatufaa. Fikirini alitikisa kichwa, ishara ya kukataa*” (Ukur 26).

Kisha Fikirini anajibu na mwandishi anadhihirisha haya kwa kusema: “Hebu niache niende zangu. Fikirini alisema huku akikurupuka ghafla kochini na kuelekea mlangoni….Fikirini aliharakisha kuufikia mlango…Kunradhi sana! Hilo sijadiriki maishani” (Ukur. 26).

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimwemwozea,* tunaambiwa kuwa Amani na Imani waliishi kwa takriban miaka miwili kama ndugu na dada yake. Hii ikimaanisha hawakujamiana kimapenzi na ilitukia kuwa mmoja akitaka kuvaa yule mwingine angetazama ukutani. Hiyo ndiyo iliyokuwa kawaida yao. Wanaendelea jinsi hii hadi wanapooana kirasmi na kupata watoto. Pia katika riwaya hii mke wa Nasaba Bora, Bi. Zuhura, anapomtega Amani ili kumvutia kimapenzi anakataa kabisa. Mwandishi anasema:

> *“Amani alipotaka kurejea kibandani mwake Bi Zuhura alimkataza. Akampa blanketi na kumwambia ajilaze kochini mle ukumbini. Wajakazi walilala katika mojawapo wa vyumba kumi na vitatu katika kasri hilo. Amani alikuwa ameparamiwa na lepe zito la usingizi Bi Zuhura alipomwita toka chumbani. “Hebu njoo uone kuna kitu hapa.” Bi Mkubwa aliita. “Sijui ni nini”. Amani akaamka haraka kwenda mlangoni pa chumba cha mwajiri wake. “Hebu ingia ndani” alisema Bi Zuhura. “Sijui ni nyoka ama nini”. Amani aliogopa. Akasitasita. Kisha akaufungua mlango na kuingia. Bi Zuhura alikuwa akisimama karibu na kitanda, kajivika gauni lake la kulalia lisilojua kuficha vya kufichwa na ambalo Amani aliwahi kuliona alipomletea mwajiri wake kitoto kiokote Uhuru”* (Ukur. 130).

Kule kuogopa kuingia chumbani mle ni ishara tosha ya msimamo wake kuelekea mahusiano ya kingono nje ya ndoa. Hii ni ithibati ya mwonoulimwengu wa mwandishi huyu kushabikia maadili ya hali ya juu kwa kutojiingiza katika mahusiano ya kingono na mtu ambaye si mwenzi wa ndoa kihalali. Kwa kuongezea haya, katika *Riwaya ya Siku Njema* mara kadhaa mhusika Kongowea Mswahili anajaribiwa kimapenzi na Fatuma lakini anakataa ikambidi Fatuma kumwachia chumba na kutafuta mahali pengine pa kulala. Mwandishi anasema:

> *“Mwishowe Amina alivua nguo zake na kuoga mle mle chumbani pasi haya. Wasio na haya wana mji wao. Nilifumba macho na kujitia hamnazo. Baada ya kuoga akajifunga kanga na kupangusa sakafu ile ya saruji kwa raka moja kuukuu…Akaingia nyuma ya pazia kulikokuwa na kitanda na kuniambia, ‘ndoo tulale. Niligutushwa mno na wito huo. Nikaingiwa na tukutiko la moyo. Huyu mwanamke ana nini? Niliwaza. Nilinyamaza kwa kitambo. Kisha akaniita tena. Kongowea jamani ndoo tulale, tumezungumza sana. Nadhani umechoka tiki. Mimi nawe tulale? Tutalala vipi? Kwani kuna ubaya gani? Sisi si maharimu….Isitoshe wewe mwenyewe ni kijana mzuri sana. Hakuna cha kutuzuia…kunalo la kutuzuia…*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

> *Litakalotuzuia ni heshima. Suala la sisi kulala pamoja halina mashiko wala murua. ….Basi tutalala kama ndugu wa kike na kiume basi. Amina tafadhali sitaki kuonekana kama mtovu wa shukrani kwa takrima yako na hisani yako. Lakini fikiria heshima yako na yangu. Nakuheshimu sana kuliko kujiheshimu mwenyewe. Najua una moyo safi. Lakini wewe na mimi ni wanadamu. Nyoyo zetu zatudanganya kuwa hatutafanya kitu. Tutalala tu. Tusidanganyike. Afadhali kutahadhari kabla ya hatari. Watu wote wangalikuwa kama wewe pasingalikuwa mwanaharamu hata mmoja"* (Ukur. 58).

Baadaye Fatuma anakiri kuwa tendo hili lilimshurutisha kuacha ile biashara yake ya ukahaba na kuanza kuuza ndizi. Pia Kongowea anapofika Kitale, msichana mmoja binti ya McDonald anamwomba wahusiane kimapenzi siku moja mamake alipoenda safari lakini alikataa kabisa hata akahamia katika kibanda kilichotengewa wafanyakazi wengine (ukur. 115). Hii ni ishara ya maadili ya hali ya juu. Hata hivyo kwa maoni ya kawaida inaonekana kuwa si halisi katika ulimwengu wa kisasa.

Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, Askari wa kwanza anasema:

> *"Nitapeleka salamu kwa dadako bila shaka kama yeye ni mzuri wa kugawa tenda na kufungasha vilivyo kama mwanamke halisi wa Kiafrika. Sivipendi visichana vya kisasa vinavyoiga Wazungu na kujikondesha vikabaki kama shingo za flamingo. Namtaka mwanamke aliyeunga sawasawa…aliyekula akashiba. Nikipata nafasi nitamtafuta huyu dadako"* (Ukur. 37).

Askari huyu alikuwa akimmezea mate Fiona akimtaka kimapenzi lakini kwa vile alimkataa anadokeza kuwa atamtafuta dadake. Hata hivyo ili kuonyesha maadili ya hali ya juu, mwandishi anatuchorea picha kupitia kwa mazungumzo kati ya Mtu wa kwanza na Mtu wa pili kwa kumkejeli Lila kuwa aliienda mjini kufanya kazi ya usekretari katika ofisi ya mawakili lakini anaishia kugombania wanaume na hivyo kumpachika jina Changudoa. Kwa kutumia maneno haya ya kukejeli na kubeza, bila shaka mwandishi anapinga tendo hili la kung'ang'ania wanaume. Kisha Matari anajaribu kumshika Fiona kwa nguvu akiwa na nia ya kumbaka lakini Fiona anapiga ukwenzi " Uwii! Uwii! Wacha kunibaka. Wacha kuniibia. Nduli wewe…kama wataka kuniua niue". Kwa hivyo Ken Walibora anamchora Fiona kama mwanamke aliyenyooka kimaadili na kufananisha tendo la kulazimishwa katika mapenzi na wizi.

### *Mwonoulimwengu wa Ken Walibora Kuhusu Udugu, Utabaka, Ubaguzi na Umataifa wa Binadamu*

Katika *Nasikia Sauti ya Mama*, Ken Walibora anasema kuwa:

> *"Iwapo palikuwa na hasama za kikabila, basi sikuhisi katika ulimwengu wangu wa utotoni. Nilichokiona ni muamana na muingiliano mwema wa kijamii. Nyoyo za watu wa makabila yote zilikuwa zimekunjuliwa kuwapokea watu wa makabila mengine. Vita nilivyowahi kuvisikia vilikuwa vya maskini na matajiri, wenye navyo na wasivyokuwa navyo na kila mmoja akipigania kusaka tonge"* (ukur. 50).

Hili linamaanisha kuwa Ken Walibora alikulia katika mazingira ya amani ambayo hayakuwa na ubaguzi na watu wote walipendana. Anazidi kusema kuwa:

> *"Mathalani nilijifunza kwamba dunia haikuwa na watu waliozungumza lugha moja. Cherengani ilikuwa na makabila tumbi nzima, si Wabukusu, si Wateso, si Wakalenjin, si Wakikuyu, si Wakisii, si Waturkana nao wote wakiwa wamebeba sehemu ya mila zao, kaida zao, mielekeo na misukumo yao, mapungukio yao na mafanikio yao….Je walihisi kuwa watu wa kabila moja la Wakenya au wanadamu? Sijui, ila nilivyoona mimi palikuwa na mwamana na itifaki njema baina ya makabila yote"* (Kur. 47-48).

Mwandishi huyu anaendeleza mwonoulimwengu huu katika kazi zake mbalimbali. Katika *Kidagaa*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

*Kimemwozea,* wahusika wanahusiana kwa njia mbalimbali bila kuuliza mtu ni wa kabila au jamii gani. Kwa mfano Amani, Imani na Dj wanapokutana wanahusiana vyema na kuwa marafiki lakini hakuna anayeuliza mwenzake kabila au jamii yake. Katika *Damu Nyeusi* mwandishi anakejeli tabia ya kubagua watu hasa kwa misingi ya rangi. Tunaelezwa jinsi Waafrika wanavyonyanyaswa na kubaguliwa hasa Fikirini, Mwafrika aliyekwenda Marekani kusoma. Akiwa huko anakutana na unyanyasaji wa hali ya juu wanaofanyiwa Waafrika. Huu ni pamoja na kuachwa na mabasi ya abiria pindi wanapokuwa pekee yao kwenye vituo vya mabasi. Hii ni kutokana na dhana ya kuwa Waafrika ni majambazi. Ubaguzi mwingine wanaofanyiwa ni katika vyombo vya kutoa haki. Mwafrika akifanya kosa linakuzwa na kupewa adhabu kubwa zaidi kuliko watu weupe. Waafrika wanakamatwa kwa makosa ambayo watu weupe hawakamatwi kama vile kuvuka barabara taa nyekundu zikiwaka. Wanapewa adhabu kali kwa makosa wanayofanya. Fikirini alitozwa faini ya dola 200 au miezi sita gerezani kwa kosa la kutofunga zipu. Mkahawani, wanatazamwa kwa dharau na wateja na wahudumu. Wanafuatwafuatwa na walinzi madukani kwa kushukiwa wataiba. Wakiwa vyuoni wanaonewa na wahadhiri wanaotoa alama kwa kupendelea watu weupe na kukandamiza wanafunzi weusi ambao hawapati shahada badala yake wanang’ang’ania kula kalenda na kukaa muda mrefu bila kuhitimu. Tunazidi kuelezwa kuwa huko Marekani watu weusi ndio wengi magerezani. Ni kama jela imeundiwa mtu mweusi. Kuhusu hili mwandishi Ken Walibora katika *Damu Nyeusi* anasema:

> *“Mkahawani, alikumbana na mitazamo ya dharau ya wateja na wahudumu ila mitazamo hiyo haikumshutua….Akaenda zake msalani kwa ajili ya haja ndogo. Alipotoka msalani aliona amekaziwa macho vibaya zaidi kuliko mwanzo. Mama mmoja mweupe alinyanyua simu yake ya mkononi na kuanza kubofya huku kamtazama Fikirini kwa jicho la uhasama. Fikirini hakuwa na mwao kuwa mama yule anampigia nani simu… Kufumba na kufumbua polisi walikuwa wamemfikia na magari yao yamesimama karibu naye, yanamemetesha taa za kuashiria dharura. Walikuwa wametoa bastola zao walizomwelekezea tayari kwa lolote….Someone called to say you are exposing yourself. Fikirini alifikishwa mahakamani na akashtakiwa kwa kosa la utovu wa adabu kwa kutofunga zipu. Jaji mweusi alimtoza faini ya dola mia mbili au kifungo cha miezi sita gerezani”* (Ukur 24).

Fikirini ananyanyaswa kwa sababu yeye ni mweusi na hivyo ni kama mada ya hadithi hii ni ya kitashtiti kwa kumwona Fikirini kuwa na damu nyeusi huku wengine Wazungu wakiwa na damu nyeupe. Kwa njia hii msimulizi anatumiwa na Ken Walibora kupinga ubaguzi wa rangi.

Kutokana na ukandamizaji na ubaguzi huo, Fikirini akajikuta anawapenda sana na kuwaamini Waafrika wenzake. Aliamini kwamba Waafrika wote ni ndugu na hivyo washikamane wakiwa ughaibuni. Pindi anapokutana na Mwafrika anamchangamkia akijua ni ndugu yake. Siku moja baada ya kuachwa na basi, Fikirini anaamua kutembea kwa miguu kwenda chuoni na hapo anakutana na mwanadada Mwafrika kwa jina Fiona. Fikirini anamwamini Fiona kuwa ni ndugu yake na Mwafrika mwenzake. Fiona akatumia fursa hiyo kumlaghai Fikirini. Alimrai Fikirini arudi ili ampeleke chuoni kwa gari lake. Fikirini anamwamini na kukubali. Alipofika nyumbani kwa mwanadada huyo anakutana na mwanaume aitwaye Bob. Bob na Fiona wanashirikiana na kumtishia Fikirini kuwa watamuua asipowapa fedha. Dada mtu ndiye aliyekazana Fikirini auawe. Hatimaye wanampora kila kitu, vikiwemo vitabu, madaftari yake na kumtupa nje uchi. Fikirini anajifunza funzo jipya. Alilazimika kujihadhari sio tu na watu weupe bali hata na ndugu zake kabisa watu weusi. Kwa njia hii Ken Walibora anapinga utabaka, ubaguzi na unafiki wa Waafrika wakiwa ughaibuni. Watu wote duniani wana damu moja na hivyo wanahitaji kuwa kama ndugu.

Katika *Nasikia Sauti ya Mama* Ken Walibora anasema:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

> *"Mama alinisisitizia umuhimu wa kutokuwa na uroho na hati nafsi. Je dunia inakuzungukia wewe tu au mvua ikunyeshee wewe mtu mmoja peke yako? ... Baadhi ya mafunzo yaliibuka ghafla nje ya shule hii aliyoniundia mama. Mathalani nilijifunza kwamba dunia haikuwa na watu waliozungumza lugha yangu tu. Cherengani ilikuwa na makabila tumbi nzima*" (Kur. 47-48).

Hapa mwandishi huyu anafunzwa kuwa na mwonoulimwengu wa kutobagua watu kwa misingi ya kikabila, rangi na tabaka. Watu wote ni ndugu.

Baadaye katika *Kidagaa Kimemwozea,* Ken Walibora anatuchorea uwepo wa matabaka mawili ya walala heri na walala hoi. Tabaka la walala heri linawakilishwa mwanzoni na wazungu wenye mali kama Major Noon au Majununi. Hawa waliishi katika maeneo yao ya kipekee na walimiliki mashamba makubwa yaliyokuwa na mimea na mifugo. Walitumikiwa na Waafrika waliozuiliwa kulima mifugo na mimea ya pesa ili wabaki maskini ndipo wawe na haja kutumikia Wazungu kwa mishahara midogo. Baadaye hasa baada ya uhuru Waafrika fulani wanaachiwa nafasi hii. Mtemi Nasaba Bora anaingia katika tabaka hili la walala heri. Aliishi katika jumba kubwa alilorithi kutoka kwa Majanuni pamoja na shamba kubwa. Tabia zake ni kama zile za Wazungu wakoloni ambao walinyanyasa na kubagua Waafrika wenzao hasa wale maskini. Aliwatumikisha wafanyakazi wake vibaya na kuwafukuza kwa hiari yake. Amani ambaye alikuwa mfanyakazi wake mwaminifu aliishi katika kibanda, alivaa matambara na kupokea mshahara mdogo huku mwajiri wake akiishi katika kasri kubwa. Tajiri mwingine Bw. Maozi anaajiri mtoto mdogo Dj ili kumchungia ng'ombe badala ya kumruhusu kuenda shuleni. Kijana huyu anasemekana kuwa na kaptura moja kuukuu na chafu. Mama ya Dj alikuwa wa tabaka la chini pia. Aliishi Madongoporomoka mtaa duni kule Songoa. Waliishi katika nyumba duni na alijiruzuku kwa kupika pombe haramu. Mwandishi analinganisha maisha ya matabaka haya mawili akiwa na nia ya kupinga hali hii.

Katika hadithi ya *Maskini Babu Yangu* katika *Damu Nyeusi* kuna utabaka wa hali ya juu unaofanya watu kuonyesha ubaguzi kwa kiwango kikubwa. Tunatambua kuwa ndoa kati ya Watantele na Wamindi na makabila mengine nchini Sakata ni nadra mno hivi kwamba ndoa ya babake na mamake msimulizi inapingwa na pande zote mbili. Msimulizi ana nywele za singasinga.Wakitembea mitaa ya Kochokocho wanavamiwa na Watantele. Walipaswa kumpeleka babu Maende kwenye vyombo vya sheria ili ibainike kama alikuwa amefanya makosa. Alisingiziwa kuiba mtoto na kumloga. Wanasikika wakisema:

> *"Mtoto Mtantele umemtoa wapi? Wee! Waacha! Unawezaje kumpata mjukuu wa Kitantele? Mchawi huyu amemroga mtoto mpaka akamwita babu yake. Mwizi wa mtoto!" Mama mmoja anamnyaka kibao shavuni na kusema "Mchomeni moto. Mwekeni tairi!"* (Ukur 79).

Kisha wanampiga Babu Maende, kumuua na kumteketeza. Haya ni madhara ya ukabila na ubaguzi. Pia inabainika wazi kuwa katika jamii hii ya Sakata kuna utabaka wa hali ya juu. Sakata ina makabila mawili tu, maskini na matajiri. Watu wenye mali wanaishi katika mitaa ya Daraja Bora wakati wale duni waliishi katika mitaa duni kama ile ya Kochokocho. Mtaa wa Madongo, eneo la Kochokocho una watu wa asili mbalimbali lakini umaskini unawafanya kuwa ndugu. Hali zao za maisha ni duni. Taswira ya nyumba zilizochakaa na kulaliana inadhihirika. Wanawake wanakaanga samaki kandokando ya barabara na kuwauzia wapita njia. Kina mama wanauza chapati zilizokaukiana na mandazi makavu. Pia kuna tofauti kati ya watu wa mjini na watu wa shambani kwani huduma bora za kijamii kama vile hospitali bora zinapatikana mijini tu. Ken Walibora anatuchorea mazingira haya kutuonyesha mwonoulimwengu wake kuwa ubaguzi si sawa. Watu wanapaswa kuwa sawa na kupokea huduma sawa kutoka kwa serikali.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

**Filosofia ya Kazi za Kuajiriwa**

Ken Walibora anaeleza kuwa amewahi kufanya kazi za ualimu, uandishi, utangazaji, kucheza mpira na kuwa afisa tawala katika idara ya magereza. Walibora anazishabikia kazi hizi katika maandishi yake kila inapowezekana na zinajitokeza kwa wingi katika kazi zake za kisanii. Kazi hizi anazofanya au kushabikia ni zile alizotagusana nazo katika maisha yake ya awali. Kwa mfano katika *Nasikia Sauti ya Mama* anataja kuhusu Gathongo jirani yao ambaye alikuwa mkongwe wa vita vya pili vya dunia. Ken anasema:

> *" Alijiliwaza kwa kulewa chakari na kutupigia gwaride uchwara left-right, left right, about turn, kana kwamba yupo jeshini bado. 'Acha kuleta chokochoko', ndivyo alivyopenda kusema sisi watoto tulipomwandama tukimkebehi na kumfanyia masihara"* (ukur. 145).

Kisa kama hiki kinajitokeza katika kazi zake nyingine za kisanii. Kwa mfano katika *Kidagaa Kimemwozea* kuna mazungumzo kati ya askari na Matuko Weye hadi Nasaba Bora anapofika katika ofisi yake ambapo tunaambiwa:

> *"Mtemi Nasaba Bora alitoka ndani na kitambi chake kilichoshiba na kutoka mbele kama cha mjamzito, kitambi kilichotishia kuivunja miguu yake ya matege." Kisha yule askari akapiga saluti tena na kuufungua mlango. "...Askari wote walikuwa wamesimama tisti. "Ndiyo afande wako ndani" alijibu yule askari. ….yule askari akakimbia kasi na kicha cha funguo alichokuwa nacho mkononi*". (Ukur 84 na 85).

Baada ya sherehe za uhuru tunapata kuwa Nasaba Bora na mkewe Bi. Zuhura:

> *"Walishikiwa miavuli na askari na kusindikizwa kuelekea garini. Askari mwingine akatokea kando akapiga saluti na kuwafungulia milango. Walipoingia akaifunga milango tena na kupiga saluti nyingine. Mtemi Nasaba Bora alipoliweka moto gari na kuondoka askari wale walikuwa wamelowa chepechepe*". (Ukur 74).

Katika ukurasa wa 72 baada ya Matuko Weye kujinyakulia jukwaa na kumkejeli Nasaba Bora tunaambiwa kuwa: "Mzee Matuko Weye aliwahiwa (na polisi) kabla ya hajalimwaya dukuduku lake lote la moyoni huku wananchi wakicheka na kumaka. Walikuja askari mikota wakambeba hobelahobela na kumtoa jukwaani".

Katika *Damu Nyeusi* mwandishi anarejelea polisi na kazi yao kwa kusema:

> *"Kufumba na kufumbua, polisi walikuwa wamefika na magari yao yamesimama karibu naye, yanamemetesha taa za kuashiria dharura. Walikuwa wametoa bastola zao walizomwelekezea tayari kwa lolote".* (Ukur 24).

Pia mwandishi anasema kupitia kwa mhusika mkuu Fikirini anayepitia mateso makuu katika mikono ya asakari polisi kwa kusema: "Kukaa kwake Marekani kumemwonyesha kuwa jela imeundiwa mtu mweusi na watu weusi wanakula kalenda katika gereza za Marekani". (Ukur 24).

Katika hadithi *Maskini Babu Yangu* kwenye ukurasa wa 76 na 77 wa diwani ya *Damu Nyeusi* Ken Walibora bado anasimulia kuhusu polisi pale msimulizi anaposema:

> *"Baba alikuwa anafanya kazi Pilka. Idili yake kwenye jeshi la polisi ilikuwa imempandisha cheo hadi kiwango cha mrakibu wa polisi. Alikuwa anahudumu katika kituo cha polisi cha Sarani, si mbali na uwanja wa mchezo wa Harambee. Tuliishi katika kambi ya polisi kwenye ghorofa ya tatu…" "Babu alifika kwetu kwenye kambi ya polisi alikotengewa chumba karibu na chumba changu".*

Masimulizi haya yanadhihirisha kuwa Ken Walibora anaelewa idara ya polisi kindani na anapenda kazi hii kwa dhati na alianza kuichangamkia akiwa mdogo na hivyo kujenga mwonoulimwengu wake.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

Kazi nyingine ambayo mwandishi huyu ameandika sana kuihusu ni ualimu. Katika *Nasikia Sauti ya Mama* anakiri mwenyewe kuwa baba yake alikuwa mwalimu. Katika shughuli zake za ualimu babake alikuwa mwenye bidii na alipenda sana kuhutubu kwenye gwaride kila siku asubuhi na jioni. Anasema kuwa:

> *"Baba akiamini hotuba zake zilikuwa nyenzo muhimu za kuadilisha, kuburudisha na kufahamisha. Hotuba zake zilikuwa sanaa iliyotokana na kipaji, idili na mazoezi na matumizi ya miaka na mikaka. Aghalabu hotuba zake zilikuwa na simulizi za ajabu alizotamba kwa maneno mateule na sauti yenye hakika na ragba, nazo zilibeba ucheshi, ukaramshi na mafunzo tele. Baba akituacha safari nyingi tumeachama kwa mshangao au kutuvunja mbavu*". (Ukur 74).

Kazi hii ya babake inamwathiri kwa kiasi kikubwa na kumfanya kusimulia mambo mengi kuhusu shule, wanafunzi, walimu na elimu. Kwa mfano katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea* anatuelezea kuhusu Mwalimu Majisifu ambaye anazembea katika kazi yake ya ualimu kiasi cha mwanafunzi wake kumlalamikia kuwa haonekani shuleni na pia anashindwa kutetea kitabu chake anachodai kuwa kakitunga cha Kidagaa Kimemwozea. Katika riwaya hii pia anatuelezea kuhusu Fao ambaye alitunga mwanafunzi wake mimba. Fao pia alifanyiwa na mtu mwingine mtihani wake wa kitaifa na kulipiwa na wazazi wake. Pia anatueleza jinsi walimu na wanafunzi wanavyojiendesha shuleni hasa kuhusiana na jinsi wanavyohusiana na wanafunzi wa jinsia tofauti. Mifano ni vile mwalimu Majisifu anavyomwambia Mashaka mpwa wake kuwa anakosa kuja shuleni ili wapate nafasi ya kuandikia wapenzi wao barua. Aidha Ken Walibora anatuchorea mhusika Mashaka anayejiingiza katika mapenzi na Ben Bella akiwa angali shuleni jambo linalomwongoza kuwehuka. Lowela binti Maozi ambaye ni mwanafunzi katika kidato cha pili anajihusisha kimapenzi na Nasaba Bora akiwa angali shuleni na kuishia kutungwa mimba na kuacha shule.

Katika Riwaya ya *Siku Njema* anatuelezea hali ya shule kule kisiwani na jinsi mwanafunzi mmoja kwa jina Kongowea alivyosababisha Selemani kuacha shule na kufungwa jela. Aidha Kongowea Mswahili anachorwa kama mhusika aliyekuwa mwerevu shuleni. Alipita mtihani wake vizuri sana na kuitwa katika shule ya upili ya kitaifa ya Buguruni kule Dar es Salaam. Hata hivyo kwa sababu ya ukosefu wa karo hakuweza kujiunga na shule hii. Baadaye akiwa Kitale anaenda kufundisha wanafunzi katika shule moja ya wasichana na hata kusaidia kumfunza binti ya Mc Donald licha ya kuwa ana kisomo cha msingi tu. (Uku 26-27).

Kazi nyingine aliyofanya mwandishi huyu kwa muda mrefu ni ya utangazaji. Ameishabikia kazi hii kwa kiasi kikubwa katika kazi zake za fasihi. Katika *Damu Nyeusi* kwenye ukurasa wa 81 akizungumza kuhusu jinsi Babu Maende alivyouawa anasema: "Wanahabari walifaidi habari ya kusambazia umma. Mpiga picha wa runinga aliyenasa tanzia ile ilipokuwa ndiyo mwanzo inaelekea kileleni alijishindia tuzo ya uanahabari bora kwa kuarifu umma kuhusu tukio hilo". Pia Fikirini anapokumbuka nchi yake anasema:

> *"Kama wakazi wengine wa Afrika Mashariki Fikirini alicheka kila aliposikia redio ya Kenya ikitangaza kauli ya baba wa taifa la Kenya Rais Daniel Arap Moi, msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi*". (Ukur 82).

Katika Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* tunaambiwa hivi kuhusu Nasaba Bora:

> *"Alianza kusoma gazeti kwanza kabla ya kuifungua barua. Ukurasa wa mbele ulikuwa na picha zilizohusiana na sherehe za sikukuu ya wazalendo. Alitafuta picha yake akaikosa. Akaamua kwamba atampigia simu mhariri wa Tomoko Leo baadaye kumuuliza kwa nini. Nduguye Mwalimu Majisifu alipokuwa mhariri wa gazeti hilo kumbe mambo yalikuwa sahali yakatawasari. Aliweza kutokea gazetini kila alipopenda…*". (Ukur 87).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

Alipokuwa katika shule ya Msingi ya St. Josephs anasema wazi kuwa alipenda kucheza mpira na hata anapoingia katika utangazaji anaanza kwa kazi ya kutangaza michezo na hasa kandanda. Anasema hivi katika Uk 62 wa *Nasikia Sauti ya Mama*;

> *"Tulikuwa twacheza kandanda, naye Emmanuel alikuwa golikipa wa timu kinzani. Nilikuwa nacheza safu ya mbele. Emmanuel alikuwa golikipa mzuri aliyechupa hewani kama samaki anavyoteleza majini. Aliweza kuzuia mikwaju mingi tuliyompigia. Mara nyingine tulipokuwa tunagawa wachezaji wa huku na huku kila mtu alimtaka upande wake".*

Baadaye katika kazi zake za kisanaa hili limejitokeza katika uandishi wake mwingi. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kwenye ukurasa wa 77 anasema: "Uwanja wa Nasaba Bora ulikuwa umezungukwa na halaiki kubwa ya mashabiki. Maashiki wa soka walikuwa wanashangilia timu zao kwa hamasa na harara". Katika *Kisasi Hapana* Kido anasema:

> *"Basi haikosi mimi na Salama tumeiga mfano wako. Yaani salama bingwa wa Riadha na mpira wa pete. Nami bingwa wa soka. Labda siku moja utasikia nikitangazwa kwenye redio, runinga au intaneti. Nikitangazwa kwa kuchezea timu ya taifa. Utasikia nikiwapiga chenga watu na kuwavisha kanzu uwanjani."* (Ukur 23).

Kwa njia hii kazi na mapenzi yake kwa soka yanachangia kujenga mwonoulimwengu wake katika maswala ya michezo.

**Nafasi ya Asasi ya Dini Katika Jamii**

Ken Walibora katika *Nasikia Sauti ya Mama* anaeleza hisia zake kuhusu dini hasa alipokuwa anakua katika shule ya msingi. Anasema:

> *"Ilimuradi nilijifunza mengi katika shule hii ya mama aliyoniwekea kama msingi wa maisha yangu ya halafu. Akieleza jinsi alivyokuwa akiomba dua awazae watoto wakue na kuwa waja waliokongowea mbele za Muumba wao na waja wenzao hali kadhalika, waja walio wacha Mungu wasiokuwa na toa wala doa". (Uku 47).*

Hili linamaanisha kuwa Ken Walibora alilelewa kuwa na mwonoulimwengu wa kidini. Katika kazi zake ametetea hili kwa njia mbalimbali. Katika *Kidagaa Kimemwozea,* mwandishi huyu anachora dini kama chombo cha kuadilisha. Babake Majisifu anawaadilisha wana wake kwa mwongozo wa Biblia na kuwausia kuwa na umoja na upendo. Hata Amani ananukuu Biblia anapoongea na Mtemi Nasababora. Anasema kuwa, kisa cha Mtemi kumshuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi ni sawa na kisa cha Yusufu na mke wa Potifa. Hata hivyo, Majisifu na nduguye Nasaba Bora wanakengeuka licha ya maadili ya dini waliyofunzwa na babao mzazi. Nasaba Bora ni mwasherati, anawadharau na kuwadhulumu watu. Majisifu naye amekuwa mraibu wa pombe hadi kifo chake. Kwa upande mwingine mwandishi anasema kuwa dini ni hifadhi ya wanafiki. Majisifu anasema kwamba ingawa dini zote zinahubiri amani, maovu mengi kama vile mauaji na vita hufanywa kwa jina la Mungu. Majisifu anaiona dini kama asasi isiyo na tumaini. Anaiona dini kama kasumba inayowalevya watu kabisa. Anaziona taasisi zote za kidini kama ombwe tupu. Nasaba Bora anaambiwa na ndugu yake jinsi makanisa mawili yalikuwa yanazozania uwanja wa kujenga kanisa. Majisifu anasema kuwa, wafuasi wa makanisa haya walipigana sana kama si askari kuingilia kati wangeuana.

Ili kuonyesha nguvu ya Biblia mwandishi anatuchorea hali ambapo Nasaba Bora anapokumbuka maovu anayotendea watu, anaagiza mke wake kumletea Biblia na kuanza kuisoma kwa sauti. Anaisoma hivyo baada ya kukumbuka jinsi alionywa na nduguye kabla ya kukengeuka. Majisifu alitakiwa na babake kwenda kusomea ukasisi kule ng`ambo, ingawa anapofika ng`ambo kusoma anabadili msimamo huo na kuachana na mpango wa kusomea dini. Pia, Imani anaponusurika kifo baada ya nyumba yao kuteketezwa, anatazama mbinguni na kusema, "Kwa nini Mungu aliruhusu dhiki kama

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

hiyo kunikuta". Majisifu kwa upande wake anapokuja nyumbani mwa ndugu yake akiwa amelewa, Mtemi anamwonya kuhusu tabia hii. Anamwambia katika uku. wa 93 kuwa "Kumbuka marehemu baba yetu alikuwa kasisi ndugu yangu na alikuwa akisema kwamba walevi hawataingia ufalme wa binguni."

Ken Walibora anatashtiti swala la dini kwa kutuonyesha kisa cha Matari ambaye ingawa anaamini kuwako kwa Mungu anamfanyia mzaha. Matari mwenyewe anasema hivi katika kur 72-73 katika tamthilia ya *Mbaya Wetu:*

> *"Nilipotoka ndani nilipita kwenye makazi ya askari polisi. Nikaona nguo kadhaa zimeanikwa nje. Wapuuzi hawa wanaanika nguo nje, hawajui zinaweza kupeperushwa na upepo wa arijojo…Nikaangalia mbele na nyuma hakuna mtu. Nikatazama kushoto na kulia, hamna mtu. Nikaangalia juu sikumwona Mungu na chini sikumwona shetani. Nikaona gunia…"*

Katika maneno haya kuna kejeli ya hali ya juu kwani Matari hamwoni Mungu kama mtu halisi anayeweza kumzuia kuiba. Mwonoulimwengu wa mwandishi hapa ni kuwa Mungu yuko ila watu wanampuuzilia tu.

## HITIMISHO

Katika makala haya tumetumia nadharia ya uhalisia kuonyesha kuwa kuna maswala katika riwaya ya *Nasikia Sauti ya Mama* ambayo ni ya kweli na yalitukia kweli katika maisha ya Ken Walibora. Mambo haya tumeyajadili kama mwonoulimwengu kutokana na kazi hii. Mwonoulimwengu huu ni kama vile utu, uongozi bora, maadili, filosofia ya kazi za kuajiriwa, udugu, utabaka, ubaguzi, umataifa wa binadamu na nafasi ya asasi ya dini. Kisha kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini tumehakiki mwonoulimwengu uliojitokeza katika *Nasikia Sauti ya Mama* na kuonyesha namna umedhihirika katika *Damu Nyeusi, Siku Njema, Kidagaa Kimemwozea, Kisasi Hapana* na *Mbaya Wetu.* Kwa kuwa mwonoulimwengu uliojitokeza wazi katika maisha halisi ya Ken Walibora kama yalivyochorwa katika tawasifu yake ya *Nasikia Sauti ya Mama* umejitokeza sana katika kazi zake za kisanaa basi inakuwa dhahiri kuwa huo ndio kweli mwonoulimwengu wa mwandishi huyu. Hii ni kwa sababu katika kazi ya fasihi, mawazo, mafunzo na falsafa ya msanii hubainisha msimamo wake kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Msimamo huu ndio hudhihirisha mwonoulimwengu wake na mwonoulimwengu ndio hufanya mwandishi au msanii wa kazi ya fasihi kuamua kufuata na kushikilia jambo fulani. Jambo hili huweza kukataliwa na wengi lakini akalishikilia tu. Mwonoulimwengu huu ndio huweza kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaoandika kuhusu mazingira yanayofanana. Tumetumia uhuru wetu wa kihakiki kufikia mkataa huu kwa kuongozwa na maoni ya Beck (1991), anayesema kuwa mhakiki ni mtu aonaye jambo kama lilivyo hasa na pia ni jaji atumiaye jicho lake kali ili atoe hukumu baada ya kusoma kazi kifasihi.

Ni wazi kuwa kwa kuelewa mwonoulimwengu wa msanii kutafanya iwe rahisi kuelewa kazi yake yoyote ya kifasihi. Kazi hii itachangia katika kufanyiza akili, kupanua uelewaji, kunoa nguvu za kufikiri, kupanua mwono, kukuza uwazaji na hisi ya ujumui ambalo ni lengo kuu la kazi yoyote ile ya fasihi. Wasomaji wa kazi za Ken Walibora watapata kuelewa kazi zake vizuri zaidi. Pia inaweza kuwa kichocheo kwa wasanii wapya ili kujua namna ya kupata maoni ya kusuka kazi zao.

### Mapendekezo

Kuelewa namna mwandishi fulani anavyousawiri ulimwengu wake kunafungua mlango kwa wahakiki kumwelewa mwandishi anayehusika na kazi zake kwa njia bora zaidi na hivyo kuwa na uwezo wa kueleza wengine mwonoulimwengu wake na falsafa anayonuia kuipitisha msanii husika. Kwa hivyo tunapendekeza kuwa:

- Jitahada ifanywe ya kuhakiki kazi za wasanii wote kwa lengo la kutambua mwonoulimwengu wa kila msanii ili kusaidia katika uelewa na uhakiki wa kazi hizo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

- Wakati wa kuhakiki kazi za msanii, wasifu na tajriba yake izingatiwe ili kumwelewa msanii mwenyewe na kazi yake vizuri zaidi na kwa njia hii kumtendea haki ya kiuhakiki.
- Wasanii watiwe moyo kuandika tawasifu zao ili kutoa mwanga kuhusu maisha yao halisi na kusaidia wasomaji wao kuelewa yale wanayosimamia.

## MAREJEO


Allen, G. (2000). Intertexuality. New York: Routledge.

American Heritage Dictionary of The English Language (2022). Boston: Houghton Mifflin.

Beck, D. (Ed). (1991). Opening the American Mind. Grand Rapids, Michigan: Baker Book House.

Coombes, H. (1953). Literature and Critism. Chatto and Windus: Australia.

Bertoncini, E. Z. (2007). A Friend in Need is a Friend Indeed: Ken Waliboras Novel Kufa Kuzikana. Katika Swahili forum 14 (153-163).

Gall, D. M., Borg, R. W., na Gall, P. G. (1996). *Education Research: An introduction* (6th ed.) New York: Longman Publishers.

Hill, C. (2O19). A Worldview Approach to Science and Scripture. Grand Rapids Michigan: Kregel Academic.

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kristeva, J. (1986). The Kristeva Reader, edited by T. Moi. Oxford: Basil Blackwell.

Leland, R. (1976). The Literature Of The Bible. Grand Rapids, Michigan: Zondervan.

Neuman, W. L. (2006). Social Research Methods Qualitative And Quantitative Approach (6th Ed). Upper Saddle River: Pearson.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: IL 61201

Raj, P. P. E. (2015). "Text/Texts: Interogating Julia Kristevas Concept of Intertextality". Research Journal of Humanities and Social Sciences 2319-7889 (3) (2015): 77-80.

Samples, K. R. (2007). A World of Difference: Putting Christian Truth-Claims to the Worldview Test (Reasons to Believe). USA: Baker Books Publishing Group.

Sire, J. W. (2010). Why Should Anyone Believe Anything at All? Westmont Illinois: Intervarsity Press.

Spirkin, A. (1990). Fundamentals of Philosophy. Moscow: Progress Publishers.

Truex, D. P. (1996). *Text Based Analysis: A Brief Introduction*. Accessed on 25 august 2023.

Walibora, K. W. (2014). *Nasikia Sauti ya Mama*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Walibora, K. W. (2014). *Mbaya Wetu*. Nairobi: Moran Publishers.

Walibora, K. W. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Spotlight Publishers (EA) Limited.

Walibora, K.W. (2010). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn publishers.

Walibora, K. W. (2008). *Kisasi Hapana. Nairobi*: Oxford University Press East Africa LTD.

Walibora, K (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Walibora, K. W. (2001). *Ndoto ya Amerika. Nairobi*: Sasa Sema Publications.

Walibora, K. W. (1996). *Siku Njema.* Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1954

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi. Phoenix Publications Ltd.

Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. New York: Penguin.